TANGAZO LA SERIKALI NA. 451 la tarehe 7/6/2024

SHERIA YA MISITU
(SURA YA 323)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 29(1))*

AMRI YA KUTANGAZA MSITU WA HIFADHI KITEMELE YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kutangaza Msitu wa Hifadhi Kitemele ya Mwaka 2024.

Tangazo

2. Eneo la ardhi ya mataji wazi ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi Kitemele.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

WILAYA YA IRINGA

MSITU WA HIFADHI KITEMELE

*Makadirio ya Eneo:* Hekta 273 au Kilometa za Mraba 2.73 Unakopatikana na Mipaka Eneo lote la ardhi ya mataji wazi awali chini ya Msitu wa Kitemele linalopatikana Wilaya ya Iringa, Mkoa wa Iringa kama lilivyochorwa katika Ramani ya Idara ya Upimaji Jb 2322 ya mwaka 1997 (Skeli 1:5,000) iliyohifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Upimaji na Ramani ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na lenye mipaka ifuatayo:

Tangazo La Serikali Na. 451 (Linaendelea)




Dodoma,
__24 Mei, 2024

ANGELLAH JASMINE KAIRUKI
*Waziri wa Maliasili na Utalii*